# Sera ya Ukusanyaji wa Madeni ya Mgonjwa

BJC Health ("BJC") na hospitali washirika wetu zinataka kukusaidia uelewe mchakato wa bili na ukusanyaji madeni na nyenzo zilizopo kwa ajili yako na familia yako.

Hospitali washirika wa BJC zitatoa huduma bila ya ubaguzi kwa hali za dharura kiafya bila ya kujali uwezo wa mgonjwa kulipa. Ikiwa una bima ya afya kama vile Medicare, Medicaid, serikali au bima nyingine ya afya, hospitali washirika za BJC zitatuma bili kwa watoa bima yako baada ya kutibiwa. Ikiwa una bima ya afya na una maswali kuhusu bima na kiwango cha manufaa yako, tafadhali wasiliana na mtoa huduma wa bima yako.

## Siku ya Huduma

Kabla au mnamo siku ya huduma, unaweza kutakiwa kulipa makadirio ya gharama zako kwa huduma utakazopata. Kama una bima, makadirio ya gharama yataamuliwa kutokana na mafao ya bima yako. Ikiwa huna bima, Amana itaombwa. Ikiwa una bima ya afya na una maswali kuhusu bima na kiwango cha manufaa yako, tafadhali wasiliana na mtoa huduma wa bima yako. Wagonjwa wasio na bima watapata punguzo la moja kwa moja la asilimia 40 kwa gharama zinazotozwa na watazingatiwa kwa msaada. Kwa kutegemea aina ya huduma na kiwango cha msaada wa kifedha, kiasi fulani cha malipo kinaweza kuhitajika. Tunaweza kukupa chati ya Kipato na Punguzo ya Sera ya Msaada wa Kifedha ambayo inaonyesha kiasi cha kulipa endapo utaomba.

## Taarifa za Malipo

Kufuatia matibabu yako, taarifa za bili zitatumwa kwako kwa kiasi chochote ambacho unaweza kuwa unadaiwa. Malipo kamili yanatarajiwa kufanywa ndani ya siku 30 za taarifa hiyo. Endapo unataka kulipa bili yako, ungependa kuweka mpangalio wa malipo, au uzingatiwe kwa msaada wa kifedha, ni muhimu uwasiliane nasi haraka kwa kupiga namba ya simu iliyoorodheshwa kwenye taarifa ya bili ili kuepuka akaunti yako kupelekwa kwa wakala wa ukusanyaji wa madeni. Pamoja na taarifa za bili, simu zinaweza kupigwa kwako kuhusiana na akaunti yako.

## Maswali Kuhusu Malipo, Migogoro au Maombi ya Bili Zilizochambuliwa

Tafadhali wasiliana nasi kwa nambari ya simu iliyoandikwa kwenye taarifa ya bili ikiwa ungependa kuuliza au kupinga bili yako.

Taarifa inayoonyesha uchambuzi wa gharama kwa huduma ulizopewa na hospitali inapatikana kwa kuombwa.

## Mpangilio wa Malipo

Iwapo huwezi kulipa salio lako kikamilifu, mipango ya malipo inapatikana kwa kiwango cha chini cha $25 kwa mwezi. Ni muhimu kuweka mpango wa malipo kupitia tovuti ya mgonjwa au kwa kutupigia kwa nambari ya simu iliyoorodheshwa kwenye taarifa yako ya bili ili kuhakikisha kuwa mipango imeidhinishwa na inatekelezwa. Kufanya malipo kidogo-kidogo bila mpango wa malipo kunaweza kusababisha akaunti yako kupelekwa kwa shirika la ukusanyaji deni.

| MWONGOZO WA MPANGILIO WA MALIPO | |
|---|---|
| **Salio la Akaunti** | **Kipindi cha Muda Mrefu Zaidi** |
| Chini ya $500 | Miezi 12 |
| $500 - $1,499 | Miezi 18 |
| $1,500 - $4,999 | Miezi 24 |
| $5,000 au zaidi | Miezi 36 |

## Wakala wa Ukusanyaji Madeni

Hospitali washirika wa BJC hutumia wakala wa ukusanyaji madeni ili kuwasaidia kukusanya malipo yaliyosalia. Malipo yaliyosalia, ambayo hayana mpangilio uliokubalika wa ulipaji, yanaweza kupelekwa kwa wakala wa ukusanyaji madeni baada ya mgonjwa kuwa ametumiwa angalau taarifa tatu za bili.

Malipo yaliyosalia ambapo barua ya kutowasilishwa imepokelewa yanaweza kupelekwa mbele kwa wakala wa ukusanyaji madeni wakati wowote wa mchakato wa ukusanyaji wa madeni. Barua za ukusanyaji zitatumwa na wakala wa ukusanyaji kwa mdaiwa husika. Zaidi ya hapo, simu zinaweza kupigwa juu ya malipo haya yaliyosalia.

Unaweza kuomba msaada wa kifedha muda wowote wakati wa mchakato wa ukusanyaji madeni, hadi siku 240 baada ya hati ya bili ya kwanza. Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu sera ya usaidizi wa kifedha ya BJC na fomu ya maombi, au kuomba kupokea taarifa iliyoandikwa au mawasiliano kielektroniki kwa kuzungumza na mwakilishi wa Huduma za Wagonjwa au kwa kupiga simu:

- BJC HealthCare kupitia namba 314-362-8400 au 855-362-8400
- Saint Luke's kupitia namba 816-932-5678 au 888-581-9401
- 417-815-8846 au 833-345-1395 kwa St. Louis Children's katika CoxHealth

Taarifa na fomu za maombi zinapatikana pia mtandaoni:

- BJC.org kwa BJC HealthCare
- SaintLukesKC.org/financial-assistance kwa Saint Luke's
- BJC.org kwa St. Louis Children's katika CoxHealth

Tafadhali jisikie huru kuulizia kuhusu msaada wa kifedha. Tuko hapa kukusaidia.

# Sera ya Ukusanyaji wa Madeni ya Mgonjwa

BJC Health ("BJC") na hospitali washirika wetu zinataka kukusaidia uelewe mchakato wa bili na ukusanyaji madeni na nyenzo zilizopo kwa ajili yako na familia yako.

Hospitali washirika wa BJC zitatoa huduma bila ya ubaguzi kwa hali za dharura kiafya bila ya kujali uwezo wa mgonjwa kulipa. Ikiwa una bima ya afya kama vile Medicare, Medicaid, serikali au bima nyingine ya afya, hospitali washirika za BJC zitatuma bili kwa watoa bima yako baada ya kutibiwa. Ikiwa una bima ya afya na una maswali kuhusu bima na kiwango cha manufaa yako, tafadhali wasiliana na mtoa huduma wa bima yako.

## Siku ya Huduma

Kabla au mnamo siku ya huduma, unaweza kutakiwa kulipa makadirio ya gharama zako kwa huduma utakazopata. Kama una bima, makadirio ya gharama yataamuliwa kutokana na mafao ya bima yako. Kama huna bima, amana itahitajika. Ikiwa una bima ya afya na una maswali kuhusu bima na kiwango cha manufaa yako, tafadhali wasiliana na mtoa huduma wa bima yako. Wagonjwa wasio na bima watapata punguzo la moja kwa moja la asilimia 40 kwa gharama zinazotozwa na watazingatiwa kwa msaada. Kwa kutegemea aina ya huduma na kiwango cha msaada wa kifedha, kiasi fulani cha malipo kinaweza kuhitajika. Tunaweza kukupatia chati ya Kipato na Punguzo ya Sera ya Msaada wa Kifedha ambayo inaonyesha kiasi cha kulipa endapo utaomba.



3259250-01-20-2026

## Taarifa za Malipo

Kufuatia matibabu yako, taarifa za bili zitatumwa kwako kwa kiasi chochote ambacho unaweza kuwa unadaiwa. Malipo kamili yanatarajiwa kufanywa ndani ya siku 30 za taarifa hiyo. Ikiwa unataka kulipa bili yako, ungependa kuweka mpangalio wa malipo, au uzingatiwe kwa msaada wa kifedha, ni muhimu uwasiliane nasi haraka kwa kupiga simu kwa namba iliyoorodheshwa kwenye taarifa ya bili ili kuepuka akaunti yako kupelekwa kwa wakala wa ukusanyaji wa madeni akaunti yako kwa shirika la ukusanyaji deni. Pamoja na taarifa za bili, simu zinaweza kupigwa kwako kuhusiana na akaunti yako.

## Maswali Kuhusu Malipo, Migogoro au Maombi ya Bili Zilizochambuliwa

Tafadhali wasiliana nasi kupitia namba ya simu iliyoorodheshwa kwenye taarifa ya bili endapo ungependa kuulizia au kupinga bili yako.

Taarifa inayoonyesha uchambuzi wa gharama kwa huduma ulizopewa na hospitali inapatikana kwa kuombwa.

## Mpangilio wa Malipo

Iwapo huwezi kulipa salio lako kikamilifu, mipango ya malipo inapatikana kwa kiwango cha chini cha $25 kwa mwezi. Ni muhimu kuweka mpango wa malipo kupitia tovuti ya mgonjwa au kwa kutupigia simu kwa namba ya simu iliyoorodheshwa kwenye taarifa yako ya malipo ili kuhakikisha kuwa mipangilio imeidhinishwa na inatekelezwa. Kufanya malipo kidogo-kidogo bila mpango wa malipo kunaweza kusababisha akaunti yako kupelekwa kwa shirika la ukusanyaji deni.



3259250-01-20-2026

| MWONGOZO WA MPANGILIO WA MALIPO | |
|---|---|
| **Salio la Akaunti** | **Kipindi cha Muda Mrefu Zaidi** |
| Chini ya $500 | Miezi 12 |
| $500 - $1,499 | Miezi 18 |
| $1,500 - $4,999 | Miezi 24 |
| $5,000 au zaidi | Miezi 36 |

## Wakala wa Ukusanyaji Madeni

Hospitali washirika wa BJC hutumia wakala wa ukusanyaji madeni ili kuwasaidia kukusanya malipo yaliyosalia. Malipo yaliyosalia, ambayo hayana mpangilio uliokubalika wa ulipaji, yanaweza kupelekwa kwa wakala wa ukusanyaji madeni baada ya mgonjwa kuwa ametumiwa angalau taarifa tatu za bili. Malipo yaliyosalia ambapo barua ya kutowasilishwa imepokelewa yanaweza kupelekwa mbele kwa wakala wa ukusanyaji madeni wakati wowote wa mchakato wa ukusanyaji wa madeni. Barua za ukusanyaji zitatumwa na wakala wa ukusanyaji kwa mdaiwa husika. Kwa kuongeza, simu zinaweza kupigwa kwa salio hizi ambazo hazijalipwa.

Unaweza kuomba msaada wa kifedha muda wowote wakati wa mchakato wa ukusanyaji madeni, hadi siku 240 baada ya hati ya bili ya kwanza. Unaweza kupata maelezo zaidi kuhusu sera ya usaidizi wa kifedha ya BJC na fomu ya maombi, au kuomba kupokea taarifa iliyoandikwa au mawasiliano kwa njia ya kielektroniki kwa kuzungumza na mwakilishi wa Huduma za Wagonjwa au kwa kupiga simu:

- BJC HealthCare kupitia namba 314-362-8400 au 855-362-8400
- Saint Luke’s kupitia namba 816-932-5678 au 888-581-9401
- 417-815-8846 au 833-345-1395 kwa St. Louis Children's katika CoxHealth

Taarifa na fomu za maombi zinapatikana pia mtandaoni:
- BJC.org kwa BJC HealthCare
- SaintLukesKC.org/financial-assistance kwa Saint Luke's
- BJC.org kwa St. Louis Children's katika CoxHealth

Tafadhali jisikie huru kuulizia kuhusu msaada wa kifedha. Tuko hapa kukusaidia.



3259250-01-20-2026